# TONE LA MWISHO

Saifu D. Kiango

## UTANGULIZI

1965 Ian Smith wa koloni la Mwingereza la Rhodesia alijitangazia uhuru wa Wazungu wachache kutokana na ukoloni wa Kiingereza. Nchi hii ambayo ilikuwa chini ya himaya ya Mwingereza hivi sasa ikawa chini ya utawala wa Wazungu wachache ambao walijinyakulia madaraka kwa njia isiyo halali na kutawala nchi hiyo kidhalimu. Uingereza nayo haikufanya lolote kurudisha utawala wa nchi hiyo chini ya himaya yake. Wananchi wazalendo walishika silaha na kupambana na utawala huu dhalimu. Utawala dhalimu uliungwa mkono na nchi za kibeberu ambapo wapiganaji wa ZIPA waliungwa mkono na nchi zinazopenda maendeleo, pamoja na nchi zilizo mstari wa mbele, katika mapambano yao ya kupigania uhuru wa kweli. Wazalendo hawa walipania kupigana hadi nchi yao iupate uhuru kweli. Tamthiliya ya Tone la Mwisho inahusu mapambano yaliyofanywa na wazalendo hawa. Ni tamthiliya ambayo inaonyesha ya kwamba udhalimu wa kikoloni ambao unaendelezwa kimabavu utaweza tu kuondolewa kwa kutumia mabavu. Tamthiliya hii inahusu ukombozi, umoja na usaliti, nafasi ya dini katika ukombozi, nafasi ya mwanamke katika ukombozi na jinsi ambavyo mapambano haya yanamjenga mwanamke mpya katika jamii. Ni tamthiliya inayohusu haki na dhuluma na unyama wa ukoloni.

E. Mbogo ameandika tamthiliya ya kihistoria yenye kuhusiana na suala la ukombozi, ambayo katika tamthiliya za dhamira hii inaikaribia Kinjeketile tu. Hii ni tamthiliya ambayo ingawaje inaihusu Rhodesia(Zimbabwe), lakini, kwa hakika inaivuka mipaka ya Zimbabwe na kuhusu sehemu nyingine za kusini mwa Afrika, na hata kuvuka mipaka ya bara hili kujumuisha nchi nyingine yoyote ile duniani ambayo inapambana na serikali ya kidhalimu.

## UDHALIMU

Serikali yoyote ile ya kidhalimu haina mizizi miongoni mwa umma. Hivyo basi itatumia kila mbinu na hila za kuhakikisha kwamba serikali hiyo inazidi kuendelea kushika madaraka. Serikali hiyo ambayo aghalabu hufanya kazi zake kwa manufaa ya watu wachache hujengeka katika misingi ya kibaguzi na hutumia mabavu ili izidi kuendelea kuwepo. Serikali inayo-

tawala katika Tone la Mwisho ni serikali ambayo imejengeka katika mfumo wa ubaguzi wa rangi. Hivyo basi askari wa serikali hiyo, pamoja na wale wa kukodiwa wanapigana ili kulinda na kutetea masilahi ya watu weupe ambao ndio walio-shika hatamu za uongozi. Kutokana na serikali hii kufuata misingi ya ubaguzi wa rangi ndiyo maana Padri anaonekana kama Mzungu ambaye ameisaliti damu yake:

| | |
|---|---|
| KOPLO ABDALA(akimvuta SAPHO): | Kwa nini humwachi huyu Mzungu? Kapteni Snow yuko wapi? |
| SOPHO: | Huyu si Mzungu Afande. Huyu ni mwendawazimu anayejaribu kusaliti damu yake!(uk. wa 16) |
| SNOW: | Sasa wewe si Mzungu? |
| PADRI: | Mzungu |
| SNOW: | Na mimi ni kama wewe siyo? |
| PADRI: | Ndiyo |
| SNOW: | Ina maana kuwa mimi na wewe tu damu moja? |
| PADRI: | Hatuzungumzi kitu kimoja. Damu unayo-isema ni tofauti na ninayosema mimi (uk. wa 19). |

Koplo Abdala anasita kumchukulia Padri hatua ya aina yoyote kwa vile yeye yu Mzungu, na Wazungu ndio wanaotawala. Katika msingi huu wa ubaguzi wa rangi Koplo Abdala ana hofu kwamba anaweza akachukuliwa hatua. Snow naye anaongea kuhusu yeye kufanana na Padri kwa maana ya kwamba wote ni Wazungu, na hivyo basi ni damu moja ambapo Padri anaona kwamba ngozi ni gamba la juu tu. Hivyo basi Snow ana mawazo ya kwamba Wazungu wote hawana budi kushirikiana pamoja dhidi ya watu weusi.

Lakini upande wa udhalimu vilevile unaungwa mkono na watu weusi wengine ambao kwa sababu wanazozijua wao wenyewe, wanapigana dhidi ya ndugu zao. Je, ndiyo kusema kuwa watu weusi hawa wanakubalika katika jamii ya watu weupe? La, hasha! Watu weusi hawa wanatumiwa tu katika kuulinda na kuuimarisha utawala huo. Zaidi ya hapo hawajulikani wala hawatambulikani. Wao wanatumiwa tu kama vyombo. Wako tayari kuua na kufa kwa ajili ya utawala dhalimu huu, ambao nao unafurahi kuwapata watu kama wao badala ya kuwapeleka watoto wao wenyewe vitani. Hivyo basi mtu mweusi anatumiwa.

kama chombo cha kumlindia mtu mweupe masilahi yake, na kupigana dhidi ya vyombo vya kimaendeleo, lakini yeye mwenyewe, kimsingi, hana manufaa yoyote anayoyapata.

Snow anamwona Padri kuwa ni Mzungu aliyekanganyikiwa kwa sababu tu yeye hakubaliani na mawazo yanayowakilishwa na serikali ya kidhalimu na kwamba anasimamia haki, ukweli na utu. Ni katika misingi hii ndiyo maana yeye hana ubaguzi wa rangi, na anawasaidia wapigania uhuru katika mapambano yao dhidi ya serikali ya kidhalimu. Yeye hafuati mkumbo uliowafumba macho Wazungu wengi bali dhamiri yake ambayo haikupotoka. Anatanguliza utu kabla ya ngozi yake:

> "Mimi ni mtu kwanza na Mzungu baadaye.
> Lazima uwe mtu kwanza kabla hujafikiri
> juu ya ngozi yako."(uk. wa 18)

Kama ilivyotajwa hapo awali utawala uliojikita kimabavu hutafuta kila mbinu za kuufanya uzidi kuendelea. Hivyo basi utawala wa aina hiyo haujali ni mbinu gani ambazo zinatumika ili kuutetea, kuulinda na kuuimarisha. Utawala wa aina hiyo utatumia mbinu za aina mbalimbali za kuwatesa wananchi wasiokuwa na hatia ili kuwaweka katika hali ya woga na kufuata amri; ili wasifikirie kufanya vitendo vyovyote vilivyo dhidi ya utawala huo; au wananchi hao waogope kuwaunga mkono watu ambao wamepania kupambana na utawala huo. Mbinu za kikatili hutumiwa ili kuwaogopesha na kuwakatisha tamaa wananchi hao.

Mbinu hizo ni pamoja na kuwaua raia kwa kuwapiga risasi na kutia sumu mimea mashambani na maji visimani:

> SNOW: Tukifika tutamwaga risasi kama mvua
> na kuua kila raia. Mimea mashambani na
> maji visimani - vyote tutatia sumu kali.
> Wakija askari wa ZIPA ama wale wa FRELIMO
> wakinywa sumu watakufa wote!(uk. wa 6)

Pamoja na hayo askari wanaopigana dhidi ya wapigania uhuru wanatumia mbinu nyingine kuwatesa watu - kuwatumbua wanawake wenye mimba eti kwa mashaka kuwa huenda wana mabomu matumboni mwao(!); na wakati mwingine askari hawa huwanajisi wanawake.

Tofauti na hali ya udhalimu na ubaguzi wa rangi ambao unatumiwa na serikali hiyo ya kidhalimu ni hali ya watu wa rangi zote kukaa pamoja bila ya kujali rangi yao; hali ya kujali ubinadamu, haki na ukweli ambayo Padri anaisimamia.

Hali hii ya kujali utu, haki na kutoangalia ngozi ya mtu ndiyo inayomfanya Padri akaonekana kuwa tofauti na Wazungu wengine.

Kinyume na hali ya udhalimu inayotawala katika Tone la Mwisho, Padri anafuata falsafa ya "Mpende jirani yako kama nafsi yako" (uk. wa 17), falsafa ambayo inakusudia kupasua kuta zilizojengwa na ubaguzi wa rangi, falsafa ambayo kama ingekuwa inafuatika basi hata huo ubaguzi wa rangi ungefutika, lakini ilivyo wadhalimu hawako tayari kufuata falsafa ya namna hiyo. Badala yake wanaitumia falsafa ya namna hiyo kwa manufaa yao wenyewe; na hivyo basi kuwaumiza watu wengine.

USALITI

Usaliti ni dhamira mojawapo ambayo inatawala katika tamthiliya hii ya Tone la Mwisho. Tamthiliya hii ina pande mbili za usaliti. Upande wa kwanza ni ule ambao wananchi wameamua kujiunga na upande wa maadui na kupigana dhidi ya wenzao ambao wanapambana ili kuupata uhuru, haki, usawa, utu, n.k. Upande huu una kina Koplo Abdala. Upande wa pili una Padri ambaye anawasaliti Wazungu wenzake kwa vile yeye ameamua kusimamia upande unaopigania haki, upande ambao katika kufanya hivyo unapambana na Wazungu ambao ndio wanaoendesha udhalimu. Padri anakataa kuungana na wadhalimu eti tu kwa vile wao ni Wazungu kama yeye!

Koplo Abdala na wenzake wameamua kuunga mkono upande wa serikali ya kidhalimu. Kwa kupigana upande wa serikali inayodumisha udhalimu askari hawa nao pia ni sehemu ya mtindo huo wa kidhalimu. Hivyo basi wanawasaliti wenzao ambao wameamua kushika bunduki na kupigana dhidi ya serikali hiyo dhalimu ili wajitoe kwenye ukoloni na wawe huru. Tsitsi anaufananisha usaliti huu na umalaya; na anauona umalaya mbaya kuliko umalaya wa wanawake:

> TSITSI: Je, mnangoja bwana wenu aje. Haijambo yule malaya wa kike. Yeye hufanya umalaya ili apate chakula, ili aweze kuishi. Bali umalaya wenu hauna kifani katika historia, na historia itawaadhibu.
>
> KOPLO ABDALA: (amechukizwa kweli kweli. Anamwendea, anamnasa kibao kimoja, viwili, tena na tena): Sasa umevuka mpaka. Malaya nani? (Kibao) Tutakunajisi, malaya mkubwa we.

TSITSI: (akizungumza kwa uchungu): Kuna malaya zaidi ya yule auzaye mwili wake, akili yake, watu wake, baba na mama yake, watoto wake. Pia na nchi yake. Kuna malaya zaidi ya huyo? (uk. wa 4)

Watu hawa wameuza pamoja na hadhi yao, kwani hata baada ya kuuza vyote hivyo wao hawana thamani yoyote, hata mbele ya ule utawala wanaoutumikia, kwani wao hawana ubora au heshima yoyote ya kibinadamu mbele ya utawala huo. Thamani yao iko tu katika utawala huo kuwatumia kufanya kazi ya hatari ambayo wao wenyewe wanasita kuwafanya watoto wao wafanye. Utawala huo dhalimu umewapa kazi hiyo kwani wao hawana thamani yoyote mbele yake.

Askari hawa ambao wanapigana dhidi ya ndugu zao sio kwamba tu wanawasaliti ndugu zao bali wanafikia hata kiasi cha kuwakana ndugu zao. Koplo Abdala anamkana shangazi yake:

MAMA: Lakini Abdala mimi ni Shangazi yako Ab...

KOPLO ABDALA (Anashika kichwa kwa mkono mmoja kama kaumwa na nyuki, anatembeatembea): Aaa! Aa! Aa! Nini?

MAMA (bado amekaa): Mimi Shangaziyo Abdala. Nilinyonya nikamtemea baba yako.

KOPLO ABDALA (anabadili sauti): Mama usinichafue. Ukome hapo hapo (Kimya) Simama upesi (MAMA anasimama).

KOPLO ABDALA: Wewe Shangazi yangu tangu lini? Umewahi kuiona sura kama hii. Wapi huko? (uk. wa 14)

Na katika uk. wa 20:

SNOW: (anabonyeza Tumbo): Hii mimba ya nani? Ya ZIPA? (wanacheka isipokuwa ABDALA).

Koplo Abdala hacheki kwa sababu anafahamu wazi ya kwamba kitendo hicho cha dharau na kashifa anatendewa shangazi yake. Ingawaje hapo mwanzoni anaukana uhusiano wake na Mama, lakini baadaye anaonyesha wazi ya kwamba hapo awali alikuwa anamkana shangazi yake.

Kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa sehemu hii Padri anaonekana kuwa msaliti, lakini wanaomwona hivyo ni wale ambao wako kwenye upande wa serikali dhalimu ambao wangemtegemea Padri kusimama kwenye upande wa Wazungu wenzake. Sapho(uk. wa 16) askari Mwafrika anayepigana upande wa serikali dhalimu anamwita Padri kuwa "mwenda-wazimu anayejaribu kusaliti damu yake." Snow naye (uk. wa 17) anamwona Padri kuwa "Yuda Iskariote." Hivyo basi itaonekana wazi kwamba upande wa Wazungu ndio unaomwona Padri kuwa msaliti, kwa kuwa tu yeye hakubaliani na udhalimu ambao unaendeshwa na Wazungu wenzake.

UMOJA

Suala la umoja ni suala muhimu katika dhamira ya ukombozi. Nchi yoyote ambayo inagombea uhuru wake haina budi kuhakikisha ya kuwa wananchi wake wanashikamana katika umoja wao. Umoja huo ni ngao thabiti katika kupigana na serikali ya kidhalimu, kama vile katika <u>Tone la Mwisho</u>. Mzee (katika uk. wa 12) anaonyesha umuhimu wa umoja wakati anapoongea na hadhira:

> MZEE(kwa hadhira): Zamani vijana walishika silaha na kutetea uhuru wa kabila lao. Vijana walikuwa na umoja ambao haukuweza kutengwa kwa radi wala mchafuko wa mawimbi ya bahari. Wakati wa vita walisahau tofauti zao wakapambana na tishio. Hungeweza kuona watu wengine wanavuka na kuingia ng'ambo ya pili...

Maneno ya Raia 1 nayo pia ni muhimu katika kuonyesha umoja uliopo miongoni mwa wana wa ZIPA:

> RAIA 1: Hata kama mkituua ni kazi bure. Sisi ni idadi ndogo tu. Ni tone moja dogo katika jumla ya wazalendo mamilioni wa Zimbabwe!!(uk. wa 14)

Mzee anaonyesha umuhimu wa umoja kama ilivyokuwa hapo zamani na Raia 1 anaonyesha uzito wa umoja katika Zimbabwe ambayo inapigana dhidi ya serikali ya kidhalimu Umoja walio nao wazalendo ndio unaowafanya wawe wajeuri mbele ya askari wa kidhalimu. Umoja huo ndio unaolipa nguvu jeshi la ZIPA kwani askari hao nao pia wanautegemea umoja huo katika kufanikisha mapambano yao. Umoja huu ni nguzo imara dhidi ya wasaliti wachache ambao wameamua kuwa vibaraka wa ukoloni na kula makombo yake.

Umoja unaozungumziwa katika Tone la Mwisho si umoja unaohusu watu wa nchi moja tu, bali ni umoja ambao unavuka nje ya mipaka ya nchi hiyo na kujumuisha nchi nyingine vilevile. Ndiyo maana Tone la Mwisho inazungumzia juu ya Frelimo na Tanzania.

> SNOW: Sisi tunajua habari zote zà FRELIMO na yule mhuni Samora Machel.
>
> KOPLO ABDALA: Wanasaidiana na Rais wa Tanzania.
>
> SNOW: Nyinyi ngoja tu. Samora na Nyerere wote tutaangusha serikali zao. Wana kimbelembele sana hawa!
>
> KOPLO ABDALA: Kweli, Kapteni. Wao wameshapata Uhuru, sasa kinawahusu nini na nchi yetu Rhodesia? (uk. wa 6)

Katika dunia hii ambayo ubeberu unajaribu kila unavyoweza ili kuzikandamiza na kuzimeza nchi nyingine, nchi hizo hazina budi kusimama pamoja na kupambana dhidi ya ubeberu. Umoja kama huu ambao unaongelewa hapa hauna budi kutiliwa mkazo. Umoja ambao unaunganisha nchi tofauti huwa ni tishio kubwa sana kwa serikali zote za kidhalimu. Ndiyo maana Koplo Abdala anauliza juu ya uhusiano baina ya hizi nchi mbili nyingine na Rhodesia kuhusu msimamo wake juu ya serikali hiyo, na jinsi ambavyo nchi hizo zilikuwa zinashawishi nchi nyingine za duniani ili zisiunge mkono utawala huo wa kidhalimu ambao nchi hizo zilisisitiza kwamba ulikuwa lazima uangushwe.

UKOMBOZI

Tamthiliya ya Tone la Mwisho imeandikwa kuzungukia dhamira ya ukombozi; dhamira hii hasa ndio kitivo cha tamthiliya yenyewe. Dhamira nyingine zote zinazojadiliwa zimejengwa kuimarisha dhamira hii kuu. Watu wa Rhodesia wanapigana na serikali ya kidhalimu ili wapate uhuru wao kamili. Watu hawa ambao wanateswa, wanaonewa na kunyanyaswa wanapigana ili waweze kuondokana na madhila yote hayo wanayoyapata. Kama anavyosema Padri(uk. wa 17) wananchi hawa wanapigana ili kuleta kile ambacho wamekataliwa kupata kwa hali ya kawaida - majadiliano:

> "...Hawa wanaomba na kupigania UHURU wao mmekataa kuwapa kwa hiari. Wameamua kupata kwa damu kwani damu yaokoa ulimwe... "

Kuna njia mbili za kugombea uhuru; moja ni ya majadiliano na nyingine ni ya mabavu. Iwapo majadiliano hayawezi kuleta mafanikio yanayotegemewa hakuna njia ila mapambano ya mtutu wa bunduki; jambo hilo limefanyika katika nchi kadha, Angola na Msumbiji zikiwa miongoni mwake; na matokeo yake yamekuwa mafanikio kwa wapigania uhuru.

Kupigania uhuru, ili kujikomboa na makucha ya ukoloni, kunadhihirisha mwamko ambao watu wameupata. Watu hawa ambao wametawaliwa na kunyanyaswa kwa muda mrefu, sasa wamefikia mahali ambapo wanasema Sasa basi:

> TONGOGARA: ...Binadamu ni binadamu. Hata ukimnyanyasa kuna kikomo chake... Na Mwafrika sasa amefikia upeo wake wa uvumilivu. Tutapigana. Tutaendelea kumwaga damu hadi tone la mwisho... (uk. wa 25)

Na mtu wa Zimbabwe sasa amefikia kikomo. Hayuko tayari tena kuendelea kukandamizwa. Ndiyo maana anapigana kujikomboa. Ukombozi anaoutaja Tongogara ni zaidi ya ule wa nchi yake. Yeye analihusisha bara zima la Afrika. Itakumbukwa ya kuwa tamthiliya hii imeandikwa katika usuli wa wakati ambao nchi nyingi za Afrika zilikuwa katika mapambano ya kupigania uhuru wake.

NAFASI YA DINI

Kabla ya ukoloni na wakati wa ukoloni dini, na hasa ya kikristo, imeonekana kama chombo ambacho kimesaidia majilio ya ukoloni na uimarikaji wake, kiasi kwamba dini haikuonekana kama chombo ambacho kingeweza kumsaidia mtu mnyonge katika matatizo yake. Viongozi wa dini wamekosa majawabu kwa matatizo ya waumini wao, na badala yake walisisitiza katika sala, kama kwamba kusali ndio tatuzi la matatizo yao yaliyowakabili. Katika tamthiliya ya Mtawa Mweusi ya James Ngugi(Ngugi wa Thiong'o) Padri anawaambia watu wasali na hali wanakabiliwa na matatizo. Sala si jawabu la matatizo yao. Katika hali kama hii waumini walikuwa na wasiwasi juu ya nafasi ya dini katika ufumbuzi wa matatizo yao.

Katika tamthiliya yake hii ya Tone la Mwisho E. Mbogo anajadili nafasi mbili za dini katika jamii. Nafasi ya kwanza ni ile inayojulikana kila mahali - dini kama chombo ambacho kinazuia maendeleo; na nafasi ya dini katika

kupambana na udhalimu. Hii nafasi ya jadi ya dini inaelezwa na Tongogara:

> "...Nyinyi wamishenari kwa miaka mingi mmesaidia kuwafunga watu wetu minyororo. Mmewafunga minyororo katika akili na mioyo yao. Leo watu wengi hawawezi kujiamini. Mmewafunza jinsi ya kugeuza shavu la pili na kusamehe... Ni hawa wamishenari wametuambia tusishughulike na mambo ya dunia hii ila tungoje kufa na kwenda mbinguni! Wazandiki wakubwa hawa!(uk. wa 23)

Katika hali kama hii waumini wamefuata dini na kujipotosha kimawazo, kwani dini haikuweza kuwapeleka mbele katika maendeleo yao. Badala yake imewafanya kuwa watiifu kwa serikali ya kikoloni; hivyo basi kujiweka katika nafasi ya kuzidi kuendelea kunyonywa.

Lakini kwa upande mwingine dini inaweza ikatumiwa katika kuleta maendeleo ya kimapinduzi katika jamii. Nafasi kama hiyo inadhihirishwa na Padri:

> SNOW: Farisayo huyu, kwa muda mrefu amekuwa anawaficha askari wa ZIPA kila wanapokwenda na kutoka Salisbury kulipua mabomu kwenye viwanda, reli, majumba ya kitalii na mali ya Wazungu wa Rhodesia. Ametoa siri zetu nyingi na kuita kikosi chetu CHINJA CHINJA (uk. wa 18).

> PADRI: Nimejitoa muhanga ili kuokoa maisha ya Waafrika, nyumba yangu imetumika kama maficho ya Wakristo waliokuwa katika hatari ya kuuawa na CHINJA CHINJA wa Smith...(uk. wa 23-24).

Padri anatumia dini kupigania haki na kweli. Yeye anasimama upande wa wapigania uhuru ambao anawasaidia. Padri huyu amejitoa mhanga kwa kuwasaidia wapiganaji au watu ambao wanasakwa na jeshi la kidhalimu la Smith. Padri anaonyesha dhahiri kwamba dini inapaswa kupigania haki. Pale ambapo watu wanaonewa na kunyanyaswa dini haina budi kuwasimamia na kuwatetea wanyonge. Dini haina budi kuwa chombo cha kuwapigania wanyonge na kuwasaidia katika harakati zao za ukombozi.

NAFASI YA MWANAMKE

Nafasi ya mwanamke ni suala jingine mojawapo ambalo E. Mbogo amelijadili katika Tone la Mwisho. Picha ya mwanzoni inayopatikana ni ile ya kumwona mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanamume. Jambo hili linajitokeza kama mara mbili hivi kwa upande wa askari dhalimu ambao wanataka kumnajisi Tsitsi na Msichana. Kwa upande wa Tsitsi, Chopa hafanikiwi, lakini, hata hivyo, Chopa anafanikiwa kumnajisi Msichana na kumwua. Hapo ni wazi kabisa kuwa Chopa amefanya hivyo ili kujistarehesha nafsi yake tu. Hapa mwanamke amechukuliwa kama chombo cha kumstarehesha mwanamume.

Picha tofauti ya nafsi ya mwanamke ni ile anayoitoa Tsitsi:

> SNOW(anamnasa kofi): ZIPA wapi?
>
> TSITSI: Nenda kawatafute(anamtemea mate).
>
> SNOW(anakasirika sana... anamchapa kofi): You bitch! Lazima utakufa. (Anaondoka pale na kutembea jukwaani kwa hasira. Askari wanamtazama kama shujaa wao, isipokuwa Mfaro peke yake). Hata wanawake, wa Kiafrika wamekuwa jeuri! Wameharibika kabisa!(uk. wa 5).

Maneno haya yanadhihirisha kuzaliwa kwa aina mpya ya mwanamke tofauti na yule mwanamke mnyonge ambaye amekuwa akifahamika wakati wote. Kutokana na hali ya mapambano kunatakikana kuwepo kwa mwanamke shupavu na aliye imara kupigana bega na mwanamume; na hali ya mapambano nayo inamjenga mwanamke wa aina hiyo. Tsitsi ni mfano wa mwanamke huyo; mwanamke ambaye ni jasiri. Katika mwanamke wa namna hii taifa lina mwanamke ambaye nafasi yake katika jamii hiyo si duni, bali ni sawasawa na ile ya mwanamume. Huyu ni mwanamke ambaye hatishiki, bali yuko tayari na ana uwezo wa kuipigania nchi yake tofauti na mawazo ambayo yamekuwa yakiiona nafasi ya mwanamke kuwa ni jikoni.

NAFASI YA JESHI

E. Mbogo katika tamthiliya yake hii vilevile amejadili nafasi ya jeshi katika jamii. Jeshi ni chombo cha dola ambacho ni cha kimabavu. Chombo hiki, kimsingi,

kimewekwa ili kuutetea na kuulinda mfumo wa utawala uliopo. Iwapo mfumo huo utatokea kuwa mfumo ambao umejengwa katika misingi ya kuwapendelea watu wachache, au tuseme kikundi fulani cha watu, basi chombo hicho nacho kitakuwepo ili kulinda masilahi ya kikundi hicho dhidi ya walio wengi. Katika hali kama hii jeshi litakuwa linatumiwa katika kuhakikisha kuwa mfumo uliopo unazidi kuendelea, na kwamba wapinzani wote wa mfumo huo wanakandamizwa, bila ya kujali maoni na malalamiko ya walio wengi; na hivyo ndivyo ilivyo kuhusu jeshi la Afrika ya Kusini ambalo linalinda mfumo na masilahi ya Wazungu wachache dhidi ya watu weusi ambao ndio walio wengi.

Katika Tone la Mwisho jeshi la serikali ya kidhalimu ya Smith linalinda na kutetea serikali ya kibaguzi ya Wazungu wachache. Hivyo basi jeshi hili linatumiwa kama chombo cha kukandamiza Waafrika, ambao ndio walio wengi, na ambao hawakusudiwi kufaidika kutokana na serikali hiyo. Zaidi ya hivyo jeshi hilo linatumika ili kupambana na wapiganaji wa ZIPA ambao wanapambana na serikali hiyo kwa minajili ya kuiangusha ili waunde serikali inayosimamia haki na ambayo itampa hadhi Mwafrika ambaye hivi sasa anadhaliliwa eti kwa vile yeye yu mweusi.

Jeshi linaweza kusimamia masilahi ya walio wengi kama tu serikali hiyo inasikiliza matakwa ya walio wengi. Hata katika hali hii vilevile jeshi linakuwa ni chombo cha kulinda serikali ambayo ina madaraka.

WAHUSIKA

Wahusika wa Tone la Mwisho wanaweza kugawanywa katika makundi mawili makubwa ambayo nayo pia yanaweza kugawanywa zaidi. Kundi moja ni lile ambalo linapigania ukombozi, ama kwa wahusika wenyewe kushiriki moja kwa moja katika mapambano hayo, au kwa kuyaunga mkono majeshi ya ZIPA ambayo yanapigana. Kundi la pili ni lile la wahusika ambao wanapigana dhidi ya wapigania ukombozi. Kundi la kwanza lina wahusika kama vile Tsitsi na Tongogara ambao wao wenyewe wanashiriki moja kwa moja katika mapambano. Halafu kuna wahusika ambao wako upande mmoja na wapiganiaji ukombozi hata kama wao wenyewe hawashiriki katika mapigano. Wahusika hawa ingawa hawashiriki katika mapigano, lakini wanashiriki katika mapambano. Katika kundi hili kuna mhusika mwingine, Padri, ambaye anawasaidia wapigania uhuru, lakini yeye kwa sababu ya rangi yake amekuwa kama mhusika

ambaye amekutwa katika njia panda. Ingawaje anawasaidia wapigania uhuru, lakini wana wasiwasi naye; wakati huohuo Wazungu wenzake wanamwona kuwa msaliti wa rangi yake kwa vile ameamua kuwa upande wa wapigania ukombozi. Kundi la pili ni lile la wahusika ambao wanapigana dhidi ya wapigania uhuru. Hawa ni askari wa upande wa serikali ambao wanapigana wakiwa na mategemeo fulani katika maisha yao, kama vile kujenga nyumba au kupata cheo. Hawa ni wasaliti. Lakini katika kundi hili vilevile kuna wahusika ambao wanaelekea kukanganyikiwa; hawajui wako upande gani. Hawa wanawakilishwa na Mfaro. Pia kuna askari wa kukodiwa, wanaowakilishwa na Kapteni Snow ambao wako tayari kupigana ilimradi wanapata fedha. Hawa hawajali upande gani ushinde; wanachotaka wao ni kulipwa tu kwa kazi yao wanayoifanya. Upande wao ukishinda au kushindwa hilo si jambo ambalo linawakera.

## Tsitsi

Ni kapteni wa jeshi la ZIPA. Mwanamke mwenye umri wa miaka 27. Yu mwanamke jasiri ambaye hata katika hali ya mateso hayuko tayari kukisaliti kikosi chake kwa kutaja mahali ambapo kipo. Anateswa ili kulazimishwa ataje mahali ambapo askari wa ZIPA wapo, lakini hayuko tayari kufanya hivyo, na badala yake anakuwa jeuri dhidi ya askari anaopambana nao. Katika uk. wa 1 Tsitsi anamjibu Koplo Abdala kwa kejeli:

> KOPLO ABDALA: Sema upesi. Wako wapi? (Kimya)
> Nasema wako wapi? (Kimya) Naona hujanyooka.
> (anamfinya na kile chuma)
>
> TSITSI (anapiga kelele). Niachilie! Niachilie!
>
> KOPLO ABDALA: Utasema!
>
> TSITSI: Ndiyo!
>
> KOPLO ABDALA (anamwachilia): Sema!
>
> TSITSI: Nyinyi endeleeni kulamba matapishi.

Pamoja na kuteswa anakoteswa Tsitsi hayuko tayari kueleza mahali ambapo wenzake wapo. Badala yake anawakejeli askari ambao wanamtesa. Na katika uk. wa 5 Tsitsi anamtemea mate Kapteni Snow:

> KOPLO ABDALA: Jeuri sana Kapteni
>
> SNOW: (Anamnasa kofi): ZIPA iko wapi?
>
> TSITSI: Nenda kawatafute (anamtemea mate).

Majibu yake ya kijeuri na yenye kejeli anayowajibu askari wanaopigana dhidi ya wapigania uhuru yanamtambulisha Tsitsi kama askari shupavu asiye mwoga na asiyekuwa rahisi kutetemeshwa wala kuyumbishwa.

Tsitsi anaona mbali zaidi kuliko kina Koplo Abdala ambao matumaini yao yote yako katika mambo madogo. Tsitsi anaona mbali zaidi na anaishi katika hali ya matumaini ya hali ya baadaye:

> TSITSI:...Haijambo yule malaya wa kike. Yeye hufanya umalaya ili apate chakula ili aweze kuishi. Bali umalaya wenu hauna kifani katika historia, na historia itawaadhibu.

Tsitsi anaishi katika hali ya matumaini ya ushindi ambao kwa vyovyote vile ni lazima upatikane. Ushindi unaweza ukachelewa kupatikana, lakini hauwezi kukosekana kabisa. Wakati fulani utapatikana na akina Koplo Abdala hawatakuwa na nafasi katika historia hiyo. Wao wataadhibiwa. Bila ya shaka Tsitsi amechukua mafunzo yake kutokana na mapambano mbalimbali ulimwenguni ambayo yamefanywa na watu wanyonge ambao wamepigania haki zao. Kwa kuwaambia hivyo akina Koplo Abdala, Tsitsi anawaambia ya kuwa wao wanapigania upande ambao kwa vyovyote vile lazima utashindwa tu; ni suala la wakati, na historia itaonyesha mwelekeo wake ulio sahihi.

Wakati Kapteni anapomwambia Tsitsi afikirie uhai wake ndipo Tsitsi anapotoa falsafa yake:

> TONGOGARA: Lakini lazima ufikirie uhai wako.
>
> TSITSI: Uhai hauna maana kwa mtu ye yote asiye na nchi. Mtumwa hana haki ya kuishi, bali kufa akipigana kuutafuta uhuru wake. (Kimya kidogo)
>
> TONGOGARA: Jaribu kusimama. (TSITSI anasimama kwa taabu)
>
> CHENJERAI: Una hakika bado una uwezo wa kuendelea?
>
> TSITSI: Katika kutafuta uhuru lazima binadamu awe tayari kupoteza vyote hata uhai wake. (uk. wa 29).

Tsitsi anayapa mapambano hadhi yake inayostahili. Binadamu yeyote anayeishi katika hali ya utumwa hana

thamani katika maisha. Atakuwa na thamani zaidi akifa katika mapambano, akiupigania uhuru wake; na binadamu anapoamua kupambana ili awe mtu huru basi hana budi kuwa tayari hata kupoteza uhai wake katika mapambano hayo.

Tsitsi ni kiwakilisho cha aina mpya ya mwanamke barani Afrika ambaye anajengeka katika hali ya mapambano. Mapambano yanamzaa mtu mpya - si mwanamke tu bali hata mwanamume, kwani kushiriki huku katika mapambano kunajenga fikra mpya katika kichwa cha binadamu. Hapa Tsitsi anachukuliwa kama uzao mpya wa mwanamke ambao unatokana na mapambano kwani uzao huu ni tofauti na ule uzao wa mwanamke ambaye anajiona na kuonekana mnyonge mbele ya mwanamume kwa vile tu yeye yu mwanamke. Mapambano haya yanawashirikisha wanawake katika shughuli ambazo hapo awali zilisadikiwa kuwa za wanaume peke yao; lakini katika mapambano haya mwanamke na mwanamume wanapambana pamoja bega kwa bega.

Tistsi ni mwanamke mwenye wadhifa wa kapteni katika jeshi la wapigania uhuru. Anapigana kuondoa dhuluma na kutaka kuleta haki na usawa katika nchi yake. Hivyo basi upiganaji wake hauna budi kuelekezwa dhidi ya tabaka tawala. Koplo Abdala na Snow ambao wanamtesa ni viwakilishi vya tabaka tawala ambao wanapigana kuutetea mfumo uliopo. Hivyo basi katika mapambano hayo Tsitsi anapambana na huu mfumo wasioutaka ambao unalindwa na akina Snow. Kutokana na hivyo msomaji anajiuliza inakuwaje basi huyu Tsitsi anasisitiza kupambana kwake yeye na Koplo Abdala na Snow. Katika msisitizo huu msomaji anapata picha kama ya kwamba Tsitsi wakati mwingine anayaweka mapambano haya katika kiwango cha watu binafsi; kwani mara kadha anazielekeza chuki zake dhidi ya Koplo Abdala na Snow.

## Kapteni Tongogara

Tongogara ni kiongozi wa jeshi la ZIPA ambalo linapigania uhuru. Yeye ndiye mwakilishi mkuu wa kile wanachokisimamia:

> TONGOGARA: Jeshi la ZIPA litapambana hadi tone la mwisho la damu, hadi Uhuru kamili wa wananchi wa Zimbabwe upatikane. Inatulazimu tuendelee kuua, na pia tuendelee kufa, kwa ajili ya heshima na haiba ya Mwafrika. Kwani katika dunia hii kuna vifo vya aina mbili: Kifo cha mtumwa na kifo cha mtu huru. Mtu huru <u>anaweza</u> kufia kitandani, lakini kifo cha

mtumwa, kifo cha mtu anayetawaliwa, mtu aliyekata shauri kuupata uhuru wake kwa mtutu wa bunduki, mtu huyo, kifo chake ni katika uwanja wa mapambano...(uk. wa 10).

Hii ndiyo azma ya chama chake - kupigana mpaka kuhakikisha ya kwamba uhuru wa kweli unapatikana. Mtu ambaye hayuko huru hana uchaguzi ila kuupigania uhuru wake na itambidi kufanya hivyo kwa gharama yoyote ile, pamoja na kupoteza maisha yake. Mtumwa mahali pake ni katika uwanja wa mapambano.

Tongogara ndiye anayetoa mkakati wa mapambano. Yeye ndiye mtu ambaye jeshi liko nyuma yake kwa uongozi wa kivita.

Tongogara ni kiongozi shupavu ambaye katika ushupavu alionao na huruma aliyonayo anaweza kufanya jambo ambalo pengine lisingeonekana kuwa la kawaida. Ndiyo maana Shamiso (uk. wa 22) anasema kuwa wakati mwingine Tongogara anaweza kuwa mtu katili asiye na huruma; au kama anavyosema Bongozozo "ana roho ngumu." Tongogara yuko tayari kufupisha maisha ya askari ambaye anateseka na anaonyesha wazi kuwa atakufa. Anafanya hivyo kwa kuwaza kwamba kama kuna hakika kuwa mtu atakufa basi hakuna haja ya kurefusha mateso na kifo chake.

Mwandishi haelezi moja kwa moja kama Tongogara anamwua mwanamke anayemzalisha(uk. wa 22) au la; lakini kutokana na maongezi ya Bongozozo, Shamiso na Chenjerai pamoja na maongezi yake mwenyewe Tongogara, ya kifalsafa, yaonyesha dhahiri kuwa amemwua huyo mwanamke ili asiendelee kuteseka; na hasa maongezi yake yanadhihirisha wazi jambo ambalo anaweza kuwa amelifanya(jambo ambalo amelifanya):

TONGOGARA: (<u>anaingia amemfunga mtoto mchanga kwa nguo za mama yake lakini mama haonekani</u>). Mapambano yanaendelea!!(<u>Kimya</u>) Mtoto wa kiume. (<u>Kimya</u>)

SHAMISO: Tutamtunzaje huyu Afande?

MAMA 4: Mama yake yuko wapi?(<u>Wote wanamtazama Mama 4 bila kumjibu</u>)

TONGOGARA: Nimefanya nini?(<u>Kimya</u>). Ulikuwa ukatili? Je, hatukupata kiumbe kipya?(<u>Kimya</u>) Upya? Uhai kuzaliwa...? Ama kutoweka? Sielewi, (<u>kimya</u>). Mbegu inakufa... hapana haifi inaoza. Lakini vipi uozo uzae kipya? Upya kutokana na uozo?

Ama uozo kutokana na upya? Kizuri kutokana na kibaya. Aaa!... Hii ni vita, na kila mzalendo yambidi kutoa mchango wake...(uk. wa 22 - 23).

Zaidi ya kuonyesha Tongogara ni mtu wa aina gani madondoo haya vilevile yanaonyesha falsafa yake. Kufa kwa huyu mwanamke kumeleta kizazi kipya - mtoto aliyezaliwa. Ukatili ambao Tongogara ameufanya ndio uliosababisha kuwepo kwa huyo mtoto ambaye amezaliwa. Pengine kama si hivyo angekufa mama na mwanawe pamoja.

Jambo linalohusu majadiliano kuhusu Tongogara ni kuhusu jinsi ambavyo analishughulikia tatizo la Padri. Tongogara anaifahamu historia mbaya yenye kuhusiana na nafasi ya dini katika Afrika. Historia hiyo ameishikilia kiasi ambacho haoni kama kiongozi wa dini anaweza kusimamia upande wa mapinduzi. Chuki aliyo nayo kuhusu dini inamfanya asitake kumsikiliza Padri kuhusu nafasi aliyo nayo katika mapambano:

PADRI: Niliwaonya wale askari wa Smith lakini hawaku...

TONGOGARA: (amepandwa na hasira. Anamwendea): Mzushi! Shetani mkubwa we! Nyinyi wamishenari kwa miaka mingi mmesaidia kuwafunga watu minyororo. Mmewafunga minyororo katika akili na mioyo yao. Leo watu wengi hawawezi kujiamini. Mmewafunza jinsi ya kugeuza shavu la pili na kusamehe. (Mateke!! Makofi!)

PADRI: Ngoja nieleze kidogo.

TONGOGARA: Unieleze kitu gani nisichokijua?...

PADRI: Nimejitoa muhanga ili kuokoa maisha ya Waafrika, nyumba yangu imetumika kama maficho ya Wakristo waliokuwa katika hatari ya kuuawa na CHINJA CHINJA wa Smith laki...(Kimya kidogo). Hawa raia wanaweza kushuhudia yaliyotokea kabla hamjafika. Wameona jinsi askari wa Smith walivyonitesa kwa ajili ya ukombozi wa Zimbabwe. Waulize raia Kapteni. (Kimya).

CHENJERAI: Je, raia ni kweli asemavyo?

TONGOGARA: Mpumbavu tu huyu!

PADRI: Waache waseme, watashindwa ilivyo kweli.

TONGOGARA: Kweli gani?

PADRI: Kwamba mimi japo ni Mzungu nimejitoa mhanga kuwasaidia watu wa Zimbabwe!

TONGOGARA: Kujitoa muhanga? Nadhani naelewa ni muhanga wa namna gani Mzungu amekuwa anaendelea kuutoa kwa Mwafrika. Je, si kwamba silaha zinaletwa pande zote mbili kwa adui na kwa ZIPA? Je, huko ni kujitoa muhanga?

PADRI: Huo ni ukweli. Mimi nauita ukweli jumla. Lakini katika ukweli huo jumla upo ukweli pekee - ukweli maalum. Ukweli unaovuka mipaka ya rangi, utaifa na dini. Huu ndio ukweli ambao umenifanya mimi nijitolee maisha yangu kwa ajili ya watu wa Zimbabwe! Kwa nini usiwaache hawa raia watoe ushuhuda? (uk. wa 23 - 24).

Chuki inayotokana na historia inaelekea kumpamba Tongogara kiasi kwamba hayuko tayari kumsikiliza sana Padri; na anamjumlisha katika kundi moja na Wazungu wengine wote; jambo ambalo laonyesha kushangaza kidogo kwa mpiganaji mwenye upeo wa Tongogara.

Inaelekea pengine msimamo alio nao kuhusu Padri si wa haki. Itakuwaje sawa kumjumlisha mtu huyu ambaye hakubaliani na Wazungu wenzake, kimsimamo, pamoja nao.

## Padri

Padri wa Tone la Mwisho ni kiongozi wa dini ambaye ameuona na kuukubali ukweli na kuamua kugombea haki na amani. Padri anasimamia haki na ukweli:

KOPLO ABDALA: Kapteni! Mtu huyu ni hatari.

PADRI: Nafurahi kwa kusikia unaniita mtu.

KOPLO ABDALA: Sio Mzungu?

PADRI: Mimi ni mtu kwanza na Mzungu baadaye. Lazima uwe mtu kwanza kabla hujafikiria juu ya ngozi yako.

SNOW(kwa kebehi): Kwa hiyo unawasaidia ZIPA kwa kuwa ni watu?

PADRI: Hiyo ni sababu kuu ya kwanza.

SNOW: Ya pili?

PADRI: Haki na kweli

SNOW: Haki na kweli Kitu gani hicho?

PADRI: Kupigania uhuru ni tendo la haki na kweli. Na Yesu alituagiza tutende yaliyo na haki na kweli mbele yake.

Katika kuipigania haki na kuupigania ukweli Padri anawaunga mkono wapigania uhuru. Katika kuupigania ukweli anajitoa muhanga na kuwasaidia Waafrika ambao wanaponea chupuchupu kuuawa na serikali ya kidhalimu. Padri anaitumia dini katika kutetea haki. Anatambua kuwa ili kuipigania haki hana budi kuangalia mbele zaidi ya upeo wa rangi, lakini suala hili laelekea kuwa na matatizo. Watu ambao wanashuhudia jinsi ambavyo Padri anateswa na askari wa Smith, ndio haohao wanaokuja kumsaliti(uk. 24). Watu hawa ambao wanafahamu wazi ukweli ukweli juu yake, hawausemi ukweli huo, na badala yake wanamuacha ateseke. Watu hawa wanamsaliti Padri kama vile ambavyo Yuda Iskariote alimsaliti Yesu:

TONGOGARA: Raia mnasemaje?

RAIA: Nyoka lazima afe!(Jogoo anawika)

PADRI: "Mara maneno ya Yesu aliyosema, 'Kabla jogoo hajawika mara mbili utakuwa umenikana mara tatu.' Raia hawa wanaukana ukweli wanaou..."

Ingawaje Raia wanaufahamu ukweli, lakini wakati wa kumhukumu Padri unapofika wanatoa hukumu iliyo dhidi yake. Watu walewale ambao amejitolea mhanga wanamsaliti. Kitendo hiki cha Raia hakieleweki. Je, kinatokana na chuki waliyo nayo ambayo inatokana na utawala wa dhuluma wa mtu mweupe, Smith, ambaye amejitwalia madaraka kwa nguvu kutoka utawala wa Kiingereza na kujitangazia uhuru?

Upande wa Wazungu nao unamwona Padri kuwa yu msaliti. Yeye badala ya kusimamia masilahi ya Wazungu wenzake

anawasaidia Waafrika katika mapambano yao. Katika kufanya hivyo Padri anafananishwa na Yuda Iskariote:

KOPLO ABDALA: Wote wanasema hawajui ZIPA walipo.

SNOW: Sio kitu. Yupo mpumbavu mmoja hapa anajua (anamwendea PADRI kwa Padri) Wako wapi ZIPA? Sema la sivyo nitakuua!

PADRI: Mpende jirani yako kama nafsi yako!

SNOW: Shit!

KOPLO ABDALA: Lakini amefanya nini huyu Padri?

SNOW: Huyu? Huyu ni Yuda Iskariote.

KOPLO ABDALA: Huyu!... Lakini... Mzungu huyu Kapteni!

SNOW: Hata baina ya Wazungu kuna wachache wanaochanganyikiwa. Anahitaji msaada huyu. (uk. wa 17).

Kwa kutokuaminiwa na upande wa wapigania uhuru na kuonekana kuwa Yuda Iskariote/na upande wa Wazungu, Padri anakuwa mhusika ambaye amekamatwa au ameshikwa kwenye njia panda - kila upande unamkataa.

Licha ya kwamba Padri anasimamia falsafa ya mpende jirani yako kama nafsi yako, pia anakubaliana na azma ya wapigania uhuru ya kutumia mtutu wa bunduki katika kufikia lengo lao:

SNOW:(teke): Unawasaidia punda wa ZIPA, ni Wazungu wenzako?

PADRI: Iliandikwa; 'Tafuteni nanyi mtaona, Ombeni mtapewa' Hawa wanaomba na kupigania UHURU wao mmekataa kuwapa kwa hiari. Wameamua kupata kwa damu kwani damu yaokoa ulimwe...

SNOW: Shut up!...(uk. wa 17)

Padri anaona kwamba wapigania uhuru wana haki na wamefanya sawa kabisa katika kushika bunduki na kupigania uhuru - haki yao. Ndiyo maana anawasaidia askari wa ZIPA:

SNOW: Farisayo huyu, kwa muda mrefu amekuwa anawaficha askari wa ZIPA kila wanapokwenda na kutoka Salisbury kulipua mabomu kwenye viwanda, reli, majumba ya kitalii na mali ya Wazungu wa Rhodesia. Ametoa siri zetu nyingi na kuita kikosi chetu CHINJA CHINJA (uk. wa 19).

Padri anapokamatwa anakutwa na silaha ambazo zimekusudiwa wapiganaji wa ZIPA. Anapigwa kutokana na mahusiano yake na ZIPA, lakini hayuko tayari kuwasaliti.

Padri anauawa na Kapteni Snow ambaye anamlenga bunduki baada ya kunyata. Padri anauawa kutokana na chuki kwamba yeye anawasaliti Wazungu wenzake ambao hakuwasaidia kwa kuwalaghai Waafrika kwa kutumia dini. Badala yake Padri anaungana nao katika mapambano yao dhidi ya utawala wa kidhalimu ambao unaendeshwa na Wazungu walio wachache katika nchi.

## Koplo Abdala

Ni mmoja kati ya askari ambao wanapigana kuilinda na kuitetea serikali ya Smith. Mawazo yake na matazamio yake yako katika kupandishwa cheo. Hivyo basi yuko tayari kufanya ukatili wowote kwa matumaini ya kufikia lengo lake. Yuko tayari kutesa na kuua watu wasio na hatia kwa matumaini ya kuwa vitendo vyake hivyo vitamfanya apandishwe cheo.

Koplo Abdala ni mtu mwenye hasira na hawezi kuuvumilia au kuupokea ukweli. Ni katika tabia yake hii ndiyo maana anamwua Mzee(uk. wa 12) ambaye anamwambia ukweli ya kwamba zamani vijana walishika silaha na kupigana kuutetea uhuru wa kabila lao, na kwamba hakuna mtu aliyewasaliti wenzake. Koplo Abdala anamwua Mzee akijua wazi kwamba amemwambia ukweli kwa vile yeye, Koplo Abdala, yu msaliti.

Koplo Abdala ni mtu katili asiyejua hata chembe ya huruma. Anaua au kuamrisha kuuawa kwa watu ambao hawana hatia. Hamwonei huruma hata shangazi yake ambaye anamkana kuwa hamjui, hali anajua vizuri sana kwamba mwanamke huyo ni shangazi yake.

Ingawaje Koplo Abdala anajionyesha kama mtu katili, lakini vilevile ni mtu mwoga. Ukatili wake anaoufanya anaufanya ili kumfurahisha Mzungu. Hivyo basi inapokuja

kwenye kumshughulikia Mzungu, Koplo Abdala anaogopa. Koplo Abdala anawaogopa Wazungu na kuwatetemekea; ndiyo maana anawakataza wenzake wasimtese Padri:

KOPLO ABDALA(anakimbia kumkataza SAPHO asimpige Mzungu): Wacha! Wacha kumpiga Mzungu, Sapho!

SAPHO: Huyu Mzungu? Huyu!(Teke, kofi!)

KOPLO ABDALA: Mwache! Snow akija utapata taabu (uk. wa 16)

Koplo Abdala ana wasiwasi kuwa Kapteni Snow hatafurahishwa na kitendo chao cha kumtenda vibaya Mzungu mwenzake; lakini baadaye anapoona kuwa Kapteni Snow naye pia yuko dhidi ya Padri, Koplo Abdala anabadilika na kumwona Padri kuwa mtu hatari. Koplo Abdala ni mtumishi mwaminifu na kibaraka aliyekamilika kwa bwana wake. Kila mara anafanya yale tu ambayo anajua yatamfurahisha bwana wake.

Koplo Abdala ana mawazo ya kufugwa na mufilisi. Haamini kuwa mtu mweusi anaweza akamshinda mtu mweupe katika vita hivi na kupata uhuru:

> "...Unadhani mimi mjinga kama nyinyi? Hiyo ZIPA inayowadanganya kila siku kwamba mtapata uhuru mbona hamjaupata huo uhuru? Mzungu kaleta maendeleo chungu nzima. Kaleta elimu, hospitali, mabarabara, ustaarabu, na kila kitu! Hata hao wanaojiita ZIPA wamesomeshwa na Mzungu. Silaha wanazotumia ni za Mzungu. Mwafrika?... Nikifuata upumbavu wenu watoto wangu watakula nini?(uk. wa 14 - 15).

Koplo Abdala anashindwa kufahamu ya kwamba maendeleo ambayo yamepatikana yanatokana na wao wenyewe. Maendeleo hayo ni jasho la watu weusi ambao wamenyonywa, na kwamba yeye anachofanya ni kutetea udhalimu na unyonyaji dhidi ya ndugu zake.

Kwa kufikiria ya kwamba ZIPA haitashinda eti kwa sababu tu inapigana na Mzungu ni kuikana historia, kwani historia inaonyesha wazi jinsi ambavyo juhudi za wananchi zimeuangusha utawala wa Kireno huko Angola na Msumbiji, na kwamba Kenya imejinyakulia uhuru wake baada ya askari wa Mau Mau kuushinda utawala wa Kiingereza. Lakini kwa vile

Koplo Abdala ana mawazo finyu na ya kibinafsi hauoni ukweli huu. Anauawa na Kapteni Tsitsi.

Farai

Ni askari anayepigana chini ya uongozi wa Koplo Abdala. Koplo Abdala anapouawa, Farai anapandishwa cheo na kufanywa kuwa koplo badala yake. Kama wahusika wengineo wanaoutetea utawala wa kidhalimu yeye pia yu mtu katili ambaye anaufanya ukatili wake kwa watu wasio na hatia ili kutaka kujikakamua na kujionyesha ya kwamba yeye ni jasiri. Anamwua mtoto mchanga eti tu kwa sababu analia. Koplo Abdala anapigana kwa matumaini ya kupandishwa cheo; Farai naye pia ana mategemeo yake kutokana na vita hivi. Yeye mategemeo yake ni kujenga nyumba ya ghorofa pindi vita viishapo.

Farai anamchekesha msomaji wakati anapomwita Tsitsi- (wapigania uhuru wote wa ZIPA) kuwa kibaraka wa ZIPA:

> "Amhoji kitu gani mwanamke mjeuri
> kama huyu! Hawa vibaraka wa ZIPA
> dawa yao ni risasi tu! Anatuambia
> sisi tunakula makombo ya Smith...
> Sisi?(anajipiga kifua). (uk. wa 2)

Yeye, Farai, na wenzake ndio vibaraka wa serikali dhalimu ambao wanawasaliti ndugu zao; na kina Tsitsi si vibaraka bali wazalendo ambao wako tayari kumwaga damu yao ili ndugu zao waweze kuishi katika hadhi na amani. Kinyume cha mambo ni kuwa Farai ambaye anajifaragua kwa kujipiga kifua anakula makombo ya Smith, kama vile anavyosema Tsitsi, ingawa Farai hataki kuukiri ukweli huo.

Farai(uk. wa 30) anaamini ya kwamba wao watashinda katika vita hivi, lakini anaposikia kuwa viongozi katika serikali ya Smith wamehamishia familia zao Ulaya na Afrika ya Kusini na wao wenyewe wanaweza kuihama nchi wakati wowote hapo tena anakuwa na wasiwasi.

> "...sisi tumesaidia sana kutetea na
> kuimarisha utawala wa Smith. Tumekuwa
> Waafrika watiifu na tumepigana kiume
> dhidi ya askari wa ZIPA. Sasa... Saa-
> Serikali ya Smith ikitoroka, utawala
> wake ukianguka sisi tutakwenda wapi?"

Farai anatambua fika kwamba kuendelea kuwepo kwao katika

utumishi kunategemea sana kuwepo kwa serikali ya kidhalimu ya Smith ambayo wao wanaitumikia kitiifu. Nguvu yao yote inategemeana(au inatokana) na Smith. Wasiwasi alio nao una msingi maana hategemei ya kwamba serikali mpya - ya ZIPA itakuwa tayari kuchukua utumishi wa watu ambao wamekuwa wakiwapinga katika juhudi zao za kuikomboa nchi yao katika kipindi chote cha mapambano.

Farai ndiye mhusika ambaye anamtilia mashaka Mfaro kwamba yu ndumila kuwili. Iwapo mawazo yake kuhusu Mfaro ni sahihi, hilo ni jambo ambalo linahitaji mjadala.

Farai anaishia kukamatwa na askari wa ZIPA, hivyo basi kudhihirisha mwisho wa kazi yake ya kuupigania, kuulinda na kuutetea utawala dhalimu wa Wazungu wachache.

## Kapteni Snow

Kiongozi wa kikosi cha jeshi la utawala wa kidhalimu ambacho kinajulikana kama CHINJA CHINJA. Yeye ndiye anayetoa mikakati ya mapambano ya kikosi hicho. Katika hali ya kutapatapa anapoona kwamba hawezi kupata habari sahihi kuhusu maeneo ya askari wa ZIPA, Snow anaamua kwenda kuteketeza vijiji vya mpaka kati ya Rhodesia na Msumbiji. Ana mipango ya kikatili ya kuangamiza raia wasiokuwa na hatia yoyote:

> "Tukifika tutamwaga risasi kama mvua
> na kuua kila raia. Mimea mashambani na
> maji visimani - vyote tutatia sumu kali.
> Wakija askari wa ZIPA ama wale wa FRELIMO
> wakinywa sumu watakufa wote! (uk. wa 6)

Ubeberu unapoona ya kwamba unashindwa kuvunjilia mbali nguvu za wananchi wapenda maendeleo uko tayari kutumia mbinu za aina yoyote ile, hata ziwe za kikatili namna gani, ili kuhakikisha ya kwamba unakwamisha juhudi na jitihada za wananchi hao. Uko tayari kufanya jambo lolote lile katika juhudi zake za kukata mkondo wa mahusiano kati ya wapiganaji wapenda maendeleo na wananchi ambao wanawaunga mkono. Utafanya kila aina ya ukatili ili kuhakikisha ya kwamba wananchi hao wanatiwa hofu na woga ili wasiendelee tena kuunga mkono jeshi la ukombozi. Na hivi ndivyo anavyofanya Snow - kuwatia wananchi woga na kuwakatisha tamaa wapigania uhuru.

Snow ni mbaguzi wa rangi ambaye anamwona Mzungu yeyote anayesimamia haki kuwa amechanganyikiwa:

SNOW: Hata baina ya Wazungu kuna wachache wanaochanganyikiwa. Anahitaji msaada huyu. (MFARO anaonyesha hasira).

SNOW: (teke): Unawasaidia punda wa ZIPA, ni Wazungu wenzako? (uk. wa 17).

Anamwona Padri kuwa mtu ambaye ameshindwa kutimiza wajibu wake:

> "Umechanganyikiwa. Mkono mmoja Biblia na wa pili bunduki. Hayaendi pamoja haya mawili. Serikali ilikutuma nje kuwafunza Waafrika waache tamaa za mwili, za dunia hii. Kuwatayarisha kwa uzima wa milele." (uk. wa 18)

Lakini hata dini haiwezi kushamiri mahali ambapo pamejaa dhuluma. Haki na amani ni mambo muhimu yanayohitajika katika kushamiri kwa dini. Kama kuna mtu ambaye amechanganyikiwa si Padri bali ni Snow. Padri anawaelewa waumini wake na kuelewa matatizo yao yanayowakabili. Yeye anafahamu wazi kuwa haki iko majaribuni, hivyo basi anapoamua kuwasaidia wapigania uhuru anasimamia upande wa haki, kinyume na Snow ambaye anasimamia udhalimu.

Snow ambaye mwanzoni ana matumaini ya kutokomezwa kwa ZIPA kutokana na kuagizwa kwa askari wa kukodiwa na silaha kutoka Afrika ya Kusini, Marekani, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani, (uk. wa 5) baadaye (uk. wa 30) anakuwa na wasiwasi mkubwa kuhusu ushindi kwa vile serikali ya Smith inaendelea kupata hasara. Pamoja na hasara ambayo serikali ya Smith inaendelea kupata, Snow anatiwa mashaka na mawazo ya dunia ambayo yako dhidi ya serikali hiyo ya kinyama na kuungwa mkono kwa majeshi ya ZIPA kwa hali na mali (uk. wa 32).

Wakati Farai anapoonyesha wasiwasi wake kuhusu maisha yao ya baadaye, baada ya ZIPA kushika hatamu za utawala, ndipo Snow anapotoa falsafa yake ya maisha:

> "(anatingisha kichwa na kuwahurumia): Askari wenzangu, lazima mwelewe kuwa, mtu kuzaliwa, anazaliwa peke yake, kuishi mnaishi wengi pamoja. Lakini kufa, lazima kila mtu afe peke yake. Hii ndiyo kanuni ya ma..." (uk. wa 33)

Hii ni falsafa ya kujaribu kukwepa wajibu. Watu hawa

wanapigania serikali ya Smith kufa na kupona, lakini inapofika kwenye kushindwa, kila kitu kinakuwa shauri yao - serikali haijali jambo gani litawatokea. Lakini pengine haiwezi kuwa falsafa ya kushangaza kwa askari wa kukodiwa ambaye njia yake ya pekee ya kumpatia kipato ni kuuza ujuzi wake.

Snow ni askari wa kukodiwa ambaye ametumia maisha yake kupigana(kwa kulipwa) katika nchi mbalimbali za Afrika - Zaire(wakati huo ikiitwa Congo), Guinea Bissau, Mozambique, Angola; sasa y'iko Rhodesia; na amekwishaitwa na Afrika ya Kusini kwenda kupigana Namibia. Yeye anapigana vita kwa minajili ya kupata fedha - hajali nani anashinda:

FARAI: Kwa nini ulikuwa unahamahama?

SNOW: Fedha! Nilikuwa natafuta fedha. Au unadhani mimi ni mwanasiasa? Ama labda unadhani nimetoka kwetu maili maelfu nyingi kuja Afrika kutetea ukoloni? Shit! What for! Mimi ni askari. Nauza ujuzi wangu ili kushibisha tumbo langu. Sijali kama Mzungu au Mwafrika anashinda vita. Sikujali majeshi ya MPLA yaliposhinda. Kwa nini basi nikose usingizi kama ZIPA watafaulu kuwaondoa Wazungu. Mimi ninachotaka ni fedha.(uk. wa 32)

Katika kupigana kwake kote Snow hajali nani anashinda katika vita hivyo. Yeye anachojali ni kulipwa gharama ya ujuzi wake tu; iwapo adui zake ndio watakaoshinda vita si jambo ambalo linaweza kumsumbua; yeye anachotaka ni fedha tu. Baada ya kushindwa kwa serikali ya Smith yeye ana mategemeo ya kwenda kupigana Namibia; lakini mategemeo yake hayo hayawezi kutekelezwa kwani Tsitsi anakatisha maisha yake.

## Mfaro

Iwapo kuna mhusika ambaye anafurahisha kwa jinsi ambavyo amechorwa vizuri ni Mfaro. Mhusika huyu hasemi maneno mengi. Wenzake wanaongea zaidi juu yake kuliko vile ambavyo yeye mwenyewe anafunua mdomo. Mfaro anafahamika kutokana na hisia zake na vitendo vyake. Mwandishi amemchora Mfaro kwa kutumia maelekezo ya jukwaa, na kumpa maneno machache sana ya kuongea. Pamoja na maneno machache aliyopewa, Mfaro anatokea kwa nguvu katika tamthiliya hii.

Mfaro ni mhusika ambaye anapigana katika upande wa askari wa utawala wa kidhalimu, lakini vitendo vyake vinaweza kuibua majadiliano kama yeye kweli yu askari mtiifu wa utawala huo ambao anaupigania na kuutetea. Msomaji anajiuliza juu ya Mfaro tokea anapokutana naye kwa mara ya kwanza kabisa(uk. wa 1) wakati ambapo anamzuia Koplo Abdala asimwue Tsitsi. Uk. wa 6 - 7 unaonyesha picha nzito zaidi kuhusu Mfaro katika uhusiano wake na Tsitsi pamoja na tabia yake:

KOPLO ABDALA: Sasa huyu mwanamke?

SNOW: Yaa! (Anafikiri kidogo). Lazima afe (anatoa kisu na kumtupia MFARO) Mfaro! (Anaonyesha ishara ya kuua kwa kisu...). O.K. Bila kele.

MFARO (ambaye kakidaka, anakikamata kisu kile kwa kusita): Sawa, Kapteni...

MFARO (sasa anamtazama TSITSI... anafikiri... anakwenda hatua moja mbele yake... halafu anaongea peke yake): Kwa nini mimi? Kwa nini nipewe kisu mimi... Kisu. Askari. Vita. (Kimya) Tunalipwa kwa kuua? (Anamgeukia Tsitsi)

TSITSI: Kama unafikiri itakusaidia.

Inaonyesha wazi jinsi ambavyo dhamiri yake imegawanyika au pengine hata tuseme imekanganyika. Kwa kuwa upande wa askari wanaoipigania na kuitetea serikali ya kidhalimu anajua wazi anategemewa kufanya kitu gani; lakini inapokuja kwenye kutekeleza kitendo chenyewe moyo wake unasita. Dhamiri yake inamshitaki. Na baadaye anaamua kwamba hawezi kumwua Tsitsi; na yuko tayari kumfungua kamba alizofungwa. Lakini anapotaka kufanya hivyo kunatokea mashambulizi naye anakimbia kuwafuata wenzake hata kabla ya kumfungua Tsitsi. Jambo hili linaonyesha jinsi alivyo mwoga na mtu asiyeweza kufikia uamuzi maalumu - amekanganyikiwa.

Mfaro ndiye askari pekee ambaye hamtazami Snow kishujaa wakati Kapteni huyo wa Kizungu anapompiga Tsitsi:

SNOW (anakasirika sana... Anamchapa kofi): You bitch! Lazima utakufa. (Anaondoka pale na kutembea jukwaani kwa hasira. Askari wanamtazama kama shujaa wao, isipokuwa MFARO peke yake)

Ndiye askari pekee ambaye hisia zake, kwa kiasi fulani(?) zinatofautiana na wenzake. Kutomtazama Snow kama shujaa wao, kama vile ambavyo wenzake wanafanya ni ishara ya kujihisi kuwa na hatia katika jambo linalotendeka. Mfaro anaihisi hali ya usaliti ambao wanaufanya kwa wenzao. Anajiwa na hisia kwamba pengine anapigana katika upande ambao asingestahili kupigana.

Wakati Tsitsi anapomtaka Mfaro amfungue kamba Mfaro anaelekea kujipinga(uk. wa 7) anapomwambia kwamba kitendo hicho kinaweza kumfanya akauawa. Tsitsi naye anampa jibu ambalo alilitoa yeye mwenyewe(uk. wa 3) "Kila mtu lazima ale udongo siku moja." Katika uk. wa 3 Mfaro anamwambia Farai "Kila mtu lazima ale minyoo siku moja." Siyo kwamba Mfaro anajipinga bali hii ni kuzidi kuhakikisha hali yake ya kukanganyikiwa.

Sehemu nyingine inayomhusu Mfaro ambayo haina budi kutupiwa jicho ni kuhusu Padri. Padri anapokamatwa Mfaro anampiga, lakini baadaye anapoufahamu uhusiano wake na wapigania uhuru ulivyo anamwangalia vinginevyo jambo ambalo linaonyesha uhusiano wake kati yake na serikali anayoipigania; na kati yake na askari wa ZIPA - ingawa jambo hili halidhihirishi uhusiano wa moja kwa moja.

Maelekezo ya jukwaa(uk. wa 20) yanatoa picha nzito kumhusu Mfaro:

> "...(KOPLO ABDALA anachukua kisu toka mfukoni na kumpa SNOW) Tutatumbua tumbo tuone kama ni toto au ina bomu la ZIPA(Raia wanapiga kelele. Askari wanajaribu kuwanyamazisha bila mafanikio. MFARO anaonyesha hasira, anakunja ngumi, anatazama bunduki yake, askari wote hawamwoni, anaiinua kidogo tu... Lakini anagundua kuwa FARAI anamwangalia... anarudisha bunduki... Wakati huo huo).

Kitendo hiki cha Mfaro kinadhihirisha chuki aliyo nayo dhidi ya wenzake ambao anapigana nao upande mmoja dhidi ya wapigania uhuru.

Mfaro si mhusika ambaye msimamo wake au tabia yake inaweza kuonekana moja kwa moja kama vile ilivyo kwa wahusika wengine. Huyu ni mhusika ambaye anaelekea amechanganyikiwa na dhamira yake inamsumbua kuhusiana na msimamo wake katika suala hili la mapambano.

LUGHA NA UCHESHI

Kwa ujumla Tone la Mwisho ni tamthiliya ambayo imeandikwa katika lugha ya moja kwa moja, yenye kueleweka kwa urahisi, na mara nyingine kuna tamathali za usemi. Kimsingi Snow ndiye mhusika ambaye wakati mwingine anatumia maneno ya Kiingereza, hasa wakati anapokasirika; na mara nyingi maneno yenyewe ama huwa ya kukashifu au kutukana. Zaidi ya maneno ya Kiingereza yanayotumika kama chombo cha mawasiliano kuna askari wa Snow ambao wanatumia maneno ya Kiingereza, lakini haya yanaelekea kuwa yale yale ambayo anayatumia Snow; hivyo basi kuonyesha jinsi gani ambavyo Snow amewaathiri. Snow amewaathiri kiasi ambacho wanarudia maneno yake, kuonyesha jinsi ambavyo watawaliwa hawa wanafugwa kimawazo na kufuata matakwa ya wakubwa wao.

Padri naye, mtu wa Mungu, anatumia sana lugha inayotokana na Biblia. Mambo mengi anayoongea anayapa tafsiri ya kibiblia au yanatokana na Biblia.

Tamthiliya ya Tone la Mwisho inajadili swali zito, lakini wakati huohuo mwandishi hakushindwa kutumia ucheshi au lugha yenye ucheshi. Katika uk. wa 15 mwandishi anatumia hali ya ucheshi kuzungumzia suala ambalo ni zito:

FARAI(kwa mama): Mama hii mimba ya nani?

MAMA: Ya kwangu.

FARAI: "Ya kwangu." Nyoo! Ulilala na shetani? Au unajifanya yule bikira wa Kiyahudi?

Bila shaka Farai anaelewa Mama ana maana gani anapotoa jibu hilo, ingawa yeye anajifanya kubabaisha kwa kuingiza hali ya ucheshi kwa kumkejeli Bikira Maria. Pengine ni jambo linalochekesha ni mwanamke anapojibu hivyo. Lakini hapa umekusudiwa ujumbe mzito. Mume wake huyu Mama amekwisha kuwa mhanga wa CHINJA CHINJA. Hivyo basi yeye amebaki peke yake kuikuza mimba yake na hatimaye kujifungua mtoto.

Padri analeta hali ya ucheshi wakati(uk. wa 25) anapojifananisha na kusalitiwa kwa Yesu:

> "Mara maneno ya Yesu aliyosema, 'kabla jogoo hajawika mara mbili utakuwa umenikana mara tatu.' Raia hawa wanaukana ukweli wanaou..."

TONE LA MWISHO

Tamthiliya ya Tone la Mwisho imepata jina lake kutokana na azma ya watu wa Zimbabwe ya kupigania utu, uhuru na hadhi yao hadi hapo watakapofanikiwa kufikia lengo lao hilo. Wako tayari hata kupigana mpaka tone la mwisho:

> TONGOGARA: Jeshi la ZIPA linapambana hadi tone la mwisho la damu hadi, Uhuru kamili wa wananchi wa Zimbabwe upatikane. Inatulazimu tuendelee kuua, na pia tuendelee kufa, kwa ajili ya heshima na haiba ya Mwafrika...(uk. wa 10).

Tongogara anaurudia usemi wa namna hii katika uk. wa 25. Tsitsi naye anasema amepigana hadi tone la mwisho. Tsitsi anakufa kishujaa, kwani yeye amekufa katika mapambano. Hakuweza kuishi kuyaona matokeo ya mapambano ambayo ameyaendesha, lakini amejitahidi kiasi chake katika kushiriki kwenye mapambano haya.

Hivyo basi jina la tamthiliya hii linakusudiwa kuonyesha nia ya wananchi wa Zimbabwe ya kupigana hadi tone la mwisho la damu hadi uhuru kamili utakapopatikana.

MASUALA MENGINE

Sehemu hii inakusudia kujadili masuala mengine ambayo yameibushwa katika Tone la Mwisho lakini hayakujadiliwa katika sehemu nyingine za makala haya. Haya ni mambo ambayo pengine hayakuangaliwa kwa undani sana, lakini ni masuala ambayo hayapaswi kupewa mgongo. Mojawapo ya masuala haya ni lile la uhusiano wa kiini na pembezoni ambao unahakikisha kuwa nchi za pembezoni(makoloni) zinatoa mazao kwa ajili ya nchi tawala ambazo baada ya kushughulikia na kuwa bidhaa, bidhaa hizo zinarudi tena katika makoloni. Makoloni yanatumiwa kama nchi za kupatia nchi tawala bidhaa ghafi kwa bei rahisi na baadaye kuzipatia nchi tawala hizo masoko kwa bidhaa zao ambazo, kwa hakika mali ghafi imetokana na nchi zinazotawaliwa. Uhusiano wa nchi hizi ni ule wa nchi inayotawala kulinyonya koloni lake. Katika uhusiano huu makoloni yamesaidia sana katika kukuza miji ya Ulaya. Jambo hili linaonyeshwa na Tongogara(uk. wa 25).

Nafasi ya Padri katika ukombozi inajitokeza waziwazi, lakini msomaji anajiuliza(uk. wa 24 chini) inakuwaje basi RAIA wanamsaliti Padri hata baada ya wao wenyewe kudhihi-

risha ukweli kuhusu upinzani wake kwa jeshi la kidhalimu na misaada yake kwa wapiganaji wa ZIPA? Kwa hakika msomaji anakanganyikiwa kuelewa inakuwaje RAIA hawa wanamfananisha Padri na nyoka; na hivyo basi kudai kifo chake? Iwapo mwandishi alikuwa na maana ya kuonyesha nafasi mbaya ambayo inachukuliwa na dini katika mapambano haya, basi itakuwa hakuchagua mhusika ambaye angeweza kumfikisha katika hatima hiyo.

Kuzaliwa kwa mtoto katika mapambano kunaonyesha alama ya matumaini kwa wapiganaji wa ZIPA. Hii ni ishara ya kuzaliwa kwa taifa jipya. Aidha ni alama ya matumaini ya kuonyesha kizazi kipya ambacho kinazaliwa. Kizazi hiki ambacho kinazaliwa katika hali ya vita kitakuzwa na kulelewa katika hali hiyo; na hatimaye kuja kuwa askari wa kulipigania jeshi la vita. Ndiyo maana mtoto huyu atabatizwa kwa matone ya damu ya watu wa Zimbabwe, kudhihirisha hali iliyomleta duniani na wajibu unaomkabili katika nchi yake.

Suala jingine ni lile la uhusiano baina ya wahusika na watazamaji wakati wa igizo. Huu ni mtindo ambao Mbogo ameutumia sana katika Giza Limeingia, lakini katika Tone la Mwisho amefanya kwa kurashiarashia tu. MZEE(uk. wa 12) wakati anapoongea juu ya umoja hazungumzi na wahusika wenzake moja kwa moja bali anaongea na hadhira ili kuwavuta karibu zaidi katika mahusiano na kunafanya wafikiri.

Tamthiliya hii inakwisha katika hali ambayo mapambano bado hayajesha, lakini yanaendelea na yanaonyesha matumaini ya ushindi.

HITIMISHO

Tamthiliya ya Tone la Mwisho ni tamthiliya inayoonyesha mapambano dhidi ya ukoloni dhalimu ambao unawatesa, kuwanyanyasa, kuwabughudhi na kuwaadhiri wananchi katika nchi yao kwenyewe. Inadhihirisha wazi kwamba ukoloni huu ambao unaendelezwa kimabavu, utaweza tu kuondolewa kwa kutumia mabavu. Mwandishi amejishughulisha na dhamira ambayo ni muhimu sana katika Afrika na nchi za dunia ya tatu kwa jumla.